USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

# MIFUMO YETU

## Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI

TOLEO NA. 10 AGOSTI 2019 — OKTOBA 2019



# Mifumo

## Katika Mikoa na Halmashauri

# Dhana ya Uimarishaji Utawala Bora na Ushirikishwaji wa Wananchi

*Mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu Mkoani Kigoma akiwa katika Zahanati ya Nyakitondo akisubiri huduma kutoka kwa wauguzi (Picha: John D. Lyimo True Vision)*

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*" Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya*

*Ofisi ya Rais-TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani"*

KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**

# Bodi ya Uhariri


## Mwenyekiti

*Mhandisi. Joseph M. Nyamhanga*
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*

## Waandishi

*Sekela Mwasubila- Kondoa Mji*
*Atley Kuni - TAMISEMI*
*Amina Rajabu– PS3*
*Wakili Mtebe– PS3*
*Jacqueline Sombe – PS3*

## Mhariri Mkuu

*Gladys Mkuchu– PS3*

## Wahariri

*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*
*Gladys Mkuchu – PS3*

## Msanifu Kurasa

*Jacqueline Sombe – PS3*



## Jarida hili hutolewa na:

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI*
*S.L.P 1923*
*Dodoma-Tanzania*
*Simu: (+255) 26 -2321234*
*Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz*
*Tovuti: www.tamisemi.go.tz*
*Blogu: blog.tamisemi.go.tz*
*Facebook: Ofisi ya Rais – TAMISEMI*
*Instagram: ortamisemi*

## Ndani ya Jarida Hili:


**Tahariri……………………………………………………………………………………........uk 6**

**FFARS Yaongeza Kasi ya Utendaji Kazi Shule ya Wasichana Kondoa…………..……....uk 7**

**GoTHOMIS Yaongeza Ufanisi katika Utoaji Huduma za Afya kwa Wakazi Nchini...…....uk 8**

**PlanRep Yawezesha Watumiaji wake Kujitathimini………………………………...…....uk 9**

**Miaka Miwili ya Tovuti za Serikali (GWF) ……………………………………………......uk 10**

**Nukuu kutoka Dawati la Wataalam…………………………………………..…….……uk 12**

## *TAHARIRI:*

# Dhana ya Utawala Bora, Ukuaji wa Teknolojia na Matumizi ya Takwimu katika kutoa Maamuzi Sahihi

Ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini, umekuwa nguzo muhimu katika kuimarisha masuala ya kijamii, kiuchumi na pia kiutamadunii. Ukuaji wa Sekta hii umechangiwa na mabadiliko ya teknolojia duniani na uhitaji wa kuimarisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati na utoaji huduma bora kwa wananchi.

Katika kuhakikisha tunakwenda sambamba na mabadiliko haya, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), tumekuwa mstari wa mbele kupitia Idara zake kusanifu mifumo kwa ushirikiano na wadau wetu wa maendeleo PS3 na kisha kutumika kuanzia ngazi za kutolea huduma,. Hadi hivi sasa kuna mifumo mikubwa inayofanya kazi hadi ngazi ya msingi ambayo imesanifiwa na wataalam wetu wa ndani.

Kuwa na mifumo ni jambo moja na matumizi ya mifumo ni jambo la pili. Kwetu TAMISEMI, mifumo imekuwa nyenzo muhimu katika masuala ya upatikanaji wa takwimu kutoka ngazi ya msingi ambazo hukusanywa na kuchakatwa kutoka sekta tofauti tofauti kama vile Elimu, Afya, Kilimo, Utawala, Mipango, Miundombinu, Maji, Ardhi, Fedha, nk. kisha kupitia Muungano Gateway mifumo huweza kubadilishana taarifa za kimfumo pamoja na upatikanaji wa takwimu.

Shabaha yakufanya hivi, ni kukuza juhudi za ugatuaji wa madaraka hadi ngazi za msingi na kusadifu dhana ya utawala bora kwa wananchi tunaowahudumia, ambapo inasisitizwa juu ya ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kuamua mambo yao kwa mustakabali wa maendeleo yao wenyewe.

Kwa upande wa pili, Ofisi ya Rais TAMISEMI, inatambua na kuheshimu matumizi sahihi ya kitakwimu kufanya maamuzi, kwakuwa katika kila mfumo zipo taarifa za kitakwimu zinazotumika kwaajili ya mipango mbalimbali ya maendeleo, mathalani Mfumo wa Tovuti ambao umeshaundiwa nyenzo maalum ya ufatiliaji ili kujua hali ya uwekaji wa taarifa mbalimbali kama vile miradi mikubwa ya maendeleo ndani ya tovuti za Halmashauri; Mfumo wa PlanRep ulioboreshwa wa kuandaa mipango ya bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambao kimsingi ili uwe na ufanisi lazima mipango yote ianzie kwa wananchi wenyewe; mfumo wa GoTHOMIS Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Vituo vya Kutoa Huduma za Afya; lakini pia mfumo wa Uhasibu na Utoaji wa taafifa za Vituo vya Kutolea Huduma FFARS, ambao unatumika kwa shughuli za kihasibu na kutoa taarifa katika ngazi ya msingi kama Shule na vituo vya kutolea huduma za Afya.

Kupitia sheria ya takwimu ya mwaka 2015, ambayo inasisitiza matumizi sahihi ya takwimu, kila Wizara na Idara za Kisekta, zinapaswa kuzingatia maelekezo na ushauri kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu juu ya mchakato na uchakataji wa taarifa za kitakwimu na mwisho kutumika kama nyenzo ya mipango ya maendeleo.

Katika toleo la 10 la Jarida la Mifumo yetu, mtaweza kusoma makala kutoka katika mifumo iliyo chini ya OR-TAMISEMI ambayo imeweza kuchambua na kuelezea kushabihiana baina ya mfumo. Dhana ya Utawala Bora lakini pia matumizi ya taarifa za kitakwimu ambazo zitatumika kama sehemu ya dira yakufanya maamuzi.

Niwatakie usomaji mwema wa Jarida hili.

**Mhandisi. Joseph M. Nyamhanga**

**Katibu Mkuu, OR -TAMISEMI**

*KUTOKA KONDOA MJI*

# FFARS Yaongeza Kasi ya Utendaji Kazi Shule ya Wasichana Kondoa

Uwepo wa Mfumo mpya wa Uhasibu na Utoaji Taarifa za Fedha katika Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS) katika Shule ya Wasichana Kondoa umeongeza hali ya utendaji kazi kwa walimu tangu kuanza kutumika kwa mfumo huo mapema Julai mosi mwaka 2017.



***Wanafunzi wa Shule ya Wasichana Kondoa wakifuatilia kwa umakini somo la mifumo katika chumba cha mifumo shuleni hapo ( Picha: Sekela Mwasubila)***

Hayo yamesemwa na Makamu Mkuu wa Shule, Mwalimu Khalifa Kinasha alipokuwa akiongea ofisini kwake juu ya hali ya utendaji kazi wa mfumo huo toka ulipoanza kutumika shuleni hapo.

”Kwa kweli mfumo huu wa FFARS umeongeza utendaji kazi kwa walimu kwani umeturahisishia sana kazi ya kuandaa taarifa za fedha tofauti na awali ambapo ilibidi mhasibu atumie muda mwingi kuandaa taarifa ya fedha na kusimamisha kazi zingine kwani shuleni hapa tunatumia mwalimu ambapo kwa sasa anatumia muda mfupi na kuendelea na kazi ya kufundisha,” anasema Kinasha.

Kinasha anaipongeza serikali kwa ubunifu wa mfumo huo ambao pia umewafanya waendelee kujifunza kompyuta kwa ukaribu zaidi hali inayowafanya waendane na kasi ya ukuaji wa teknolojia unaoendelea duniani ambao unafanya mambo mengi kwa njia ya kidijitali na kurahisisha utendaji kazi.

Hata hivyo anaishauri serikali kuendelea kubuni mifumo mingine mizuri ili kupunguza tatizo la kuwa na takwimu tofauti na hali halisi mashuleni hasa za walimu na wanafunzi hali ambayo pia itapunguza kwa kiasi kikubwa migogoro kati yao na viongozi kwani watakuwa na takwimu sawa.

Kwa upande wake Kaimu Mhasibu wa shule Mwalimu Mustafa Nkondokaya anaongeza kuwa kwake mfumo huo umekuwa ni msaada mkubwa sana kwani amekuwa akiandaa taarifa ya fedha kwa umakini na uhakika zaidi tofauti na awali ambapo taarifa zilikuwa zinatofautiana wakati wa uandaaji.

Anaendelea kueleza kuwa mfumo pia umemsaidia wakati wa kuandaa malipo kwani hujua chanzo cha fedha moja kwa moja na kumlazimisha kutumia fedha kwa kigezo kilichopo kulingana na bajeti iliyopangwa ambapo awali alikuwa akitumia fedha bila kujua chanzo na bila kufuata bajeti na kusababisha shule kutumia fedha nyingi bila sababu.

“Mfumo umenirahisishia kazi pia ya utunzaji wa kumbukumbu za taarifa ya fedha na kunifanya niweze kuangalia salio la benki popote nilipo na kwa wakati wowote hivyo napata muda mwingine wa kuendelea na majukumu mengine ya ufundishaji.” Anasema Mustafa

Aidha anafafanua zaidi kuwa uwazi umeongezeka katika masuala ya fedha kwani ngazi mbalimbali wanaweza kuangalia mfumo mzima wa makusanyo na matumizi ambapo awali iliwalazimu kwenda kupeleka taarifa hizo kwa gharama pale zinapohitajika na hali hii imepunguza ubadhilifu kwa kiasi kikubwa kwa watumishi wasio waaminifu.

Mfumo wa FFARS ulianza kutumika Julai 2017 kwenye zahanati, vituo vya afya, hospitali na shule ili kuboresha usimamizi wa fedha za umma kwa kutumia njia ya kielektroniki.

***Sekela Mwasubila- Kondoa Mji***

*KUTOKA MTWARA NA MARA*

# GoTHOMIS Yaongeza Ufanisi Katika Utoaji Huduma za Afya kwa Wananchi

Kabla ya uwekaji wa Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Vituo vya Kutolea huduma za Afya (GoTHOMIS) katika Kituo cha Afya Dinyeche katika Halmashauri ya Mji Nanyamba, Mkoani Mtwara kulikuwa na utunzaji wa kawaida wa mafaili ya taarifa za wagonjwa, uchelewashaji wa huduma kwa wateja. Taarifa zilikuwa zinawekwa kwenye makabati ambapo jambo hili limekuwa likipoteza muda sana hivyo kutoa huduma kwa wateja wachache.

Uwekaji kumbukumbu wa taarifa za dawa ulikuwa kwa kutumia karatasi (manual) madaktari hawakuwa na uelewa wa dawa gani zipo stoo na zipi hazipo na hivyo mgonjwa anaweza akaandikiwa dawa na daktari lakini akifika kwenye duka la dawa la kituo, dawa hizo zinakuwa zimeisha. Kuna muda inawalazimu wagonjwa kwenda kununua dawa nje ya kituo.

Daktari Peter Kyaborati ambaye ni Mganga Mfawidhi wa Mji anasema “mfumo wa GoTHOMIS umesaidia katika kusimamia vizuri ukusanyaji wa ada za wateja na kirahisi kabisa tunaweza kugundua watumishi wanaofanya ubadhilifu katika utoaji wa dawa kwa wagonjwa.”



*Mhudumu wa Maabara akitoa huduma kwa mkazi wa Nyamongo kwa kutumia mfumo wa GoTHOMIS katika Kituo cha Afya Nyamongo (Picha : Wakili Mtebe, PS3)*

Vilevile tangu kuwekwa kwa mfumo mwezi Julai 2018 ,kumekuwa na mabadiliko makubwa sana katika ukusanyaji wa ada za wagonjwa ambapo ukusanyaji ulikuwa ni shilingi 4,900 kwa siku, lakini baada ya kuweka mfumo, ukusanyaji umeongezaka hadi kufika 130,000 kwa siku ambapo fedha hizo zinatumika kununua vifaa tiba, madawa na kuboresha miundombinu hivyo kuboresha huduma kwa wakazi wa eneo hilo.



*Picha ikionesha uwekaji wa awali wa majalada ya wagonjwa katika Kituo cha Afya Dinyeche (Picha: Amina Rajabu, PS3)*

Kwa upande wake Daktari Rasuli Said kutoka Kituo cha Afya cha Nyomongo kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Tarime Mkoani Mara anasema “kufanya kazi katika mfumo wa kielektroniki kumetengeneza mazingira mazuri ya kazi kwa watumishi na kumechangia sana kuwepo na utoshelevu wa utoaji wa huduma, hivyo kupunguza sana malalamiko ya wananchi.”

“Mbali na kwamba kuna uhahaba wa watumishi kituoni, mfumo unatuwezesha kusimamia kazi kwa kiwango kikubwa na kwa kushirikiana na Maafisa kutoka TAMISEMI na Mradi wa PS3 hapa Mara ambao hufika mara kwa mara kwaajili ya kujenga uwezo kwa watumishi wapya ambao hufika kutekeleza majukumu hapa Nyamongo”, anaongeza Dr. Rasuli.

Naye mkazi wa Nyamongo Mzee Chacha Mwita anasema, “sasa hatutembei na mafaili yetu ya wagonjwa kutoka chumba kimoja hadi kingine, majina yetu na taarifa nyingine zinapatikana katika mtandao.”

Kwa sasa Wakazi wa Nyamongo wananufaika mojamoja na utumiaji wa Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Vituo vya Kutolea huduma za Afya.

***Amina Rajabu na Wakili Mtebe—PS3– Mtwara na Mara***

*KUTOKA KONGWA*

# PlanRep Yawezesha Watumiaji wake Kujitathimini

Mchakato wa upitiaji wa bajeti katika ngazi ya Halmashauri umekuwa ni zoezi ambalo limewafanya watumishi kutumia muda mrefu kutokana na zoezi hilo kufanyika kwa njia ya kawaida hivyo kufanya watumishi kutofanya kazi zao kwa ufasaha na kwa wakati.



*Mkufunzi wa Kitaifa wa Mfumo wa PlanRep Salum Dhamini wakati wa moja ya mafunzo ya Mfumo wa PlanRep iliyoboreshwa (Picha: Jacqueline Sombe, PS3)*

Suala hili lilikuwa likisababisha Halmashauri nyingi kuitwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR– TAMISEMI) kwa ajili ya kufanya mapitio upya ya bajeti zao kabla hazijapitishwa.

Hivi karibuni, OR- TAMISEMI kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya sekta za Umma (PS3) wamefanikiwa kuendelea kuboresha Mfumo wa Mipango, Bajeti na Taarifa (PlanRep) kwa kuufanya mfumo huo kuwezesha watumiaji kufanya kazi kwa kusaidiana.

Meneja wa Mifumo kutoka PS3, Revocatus Mtesigwa anaeleza kuwa mfumo huu unawawezesha watumiaji wake kujitathimini wakati wa maandalizi ya bajeti katika ngazi za vituo vya kutolea huduma.

Anasema kabla ya kufanya bajeti mtumiaji anao uwezo wa kujitathimini na kujihakikishia kama bajeti ni sawa (*SMART*) na kama imekidhi ukomo (*ceiling*) uliowekwa.

"Katika maboresho haya ya mfumo wa PlanRep, kabla ya kufika tamati ya bajeti, mfumo haukubali mtumiaji kufunga hadi uhakikishe mtumiaji amemaliza au kufikia ukomo (*ceiling*) na unaweza kukuonesha pia asilimia uliyofikia katika ujazaji wa bajeti na endapo mtumiaji atamaliza kuingiza taarifa ndipo mfumo utamkubalia mtumiaji aweze kufunga." Anaongeza Bw. Mtesigwa.

Vilevile Mtesigwa anaeleza kuwepo kwa "*automation process review*" ambayo ni mbinu ya kutumia mifumo katika uendeshaji wa kazi mbalimbali na hivyo kupunguza mchango wa binadamu (*human intervention*) kwa kiasi kikubwa na kuipa mifumo uwezo kufanya kazi yenyewe kwa msaada mdogo wa mtalaam au mtumiaji wa mfumo.

Anafafanua kuwa kuna baadhi ya Halmashauri zilikuwa zinashindwa kufikisha kazi zao kwa muda muafaka hasa kwa upande wa afya ambapo bajeti zao zilikuwa kubwa kiasi kwamba kuwachukua zaidi ya mwezi mmoja kuandaa bajeti hizo.

"Mfumo unafanyiwa maboresho mara kwa mara na kwa sasa unafanikisha kuwepo kwa mrejesho wa papo kwa papo katika ngazi zote za mfumo," anasema Mtesigwa

Wakati huohuo Afisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Salum Dhamini anasema kuwa mfumo wa PlanRep unaleta ujumbe kwamba kazi uliyoifanya imeenda mahali husika. Mfano FFARS kutoka kwenye planRep, pia kama sehemu (*segment*) ambayo umeingiza mfumo haijaenda mahali husika au haijafika. Mfumo unakupa mrejesho kwamba ni sababu gani sehemu *(segment)* hiyo haijafika ulikotuma hivyo kukupa nafasi ya kuweza kufanya marekebisho au maboresho.

Anaongeza kuwa mtumiaji anaweza kujitathimini na kuwepo kwa mrejesho katika mfumo *(Automatic reply/alert)* na pia una vipengele (*features*) vya kipekee vinavyomuwezesha mtumiaji kutofautisha mawazo (*comments)* ya watumiaji tofauti wa mfumo.

Upitiaji wa bajeti kielektroniki una faida nyingi katika utumiaji wa mitambo inayojiendesha yenyewe (Automation) kama vile utoaji wa taarifa bora, matumizi mazuri ya rasilimali, usalama wa taarifa na usalama wa wafanyakazi ambao walikuwa wakisafiri kwa mwendo mrefu kila muhala/msimu wa bajeti.

***Jacqueline Sombe- PS3***

## MAKALA MAALUM

# Miaka Miwili ya Tovuti za Serikali (GWF)

- ***Je, Tovuti za Mikoa, Halmashauri ni Majokofu au Magofu ya Habari?***

Mfumo wa Tovuti za Serikali (*Government Website Framework-GWF*) kwa Mikoa na Halmashauri nchini umetimiza miaka miwili na miezi minne tangu kuboreshwa kwake tarehe 27 Machi, 2017. Mfumo huu ulizinduliwa na aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. George Simbachawene.

Pamoja na jitihada zilizofanywa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo nchini USAID kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma ( *Public Sector Systems Strengthening PS3)* kwa kuziwezesha Halmashauri zote 185 na Mikoa 26 ya Tanzania Bara kuwa na tovuti. Wadau wengi wakati na baada ya tukio la uzinduzi wa tovuti hizo wamekuwa wakijiuliza maswali mawili ya msingi kuwa Je, tovuti hizo zitakuwa majokofu ya kuhifadhi dhana ya utawala bora kwa kuongeza mapana ya kuhabarisha umma au magofu yaliyotelekezwa baada ya ujenzi?

Denis Gondwe Afisa Habari katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma anakiri kuwa, dhana ya gofu imetoweka na kuwa Jokufu la Habari.

“Mfumo wa *GWF* umekuwa msaada mkubwa katika kufikisha habari na ajenda za Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa wananchi wake. Hili limejidhihirisha kufuatia muitikio mkubwa wa wananchi kwenye zoezi la uuzaji wa viwanja kwani watembeleaji wa tovuti kutoka ndani na nje ya nchi wamekuwa wakisoma habari na matangazo tunayotangaza kupitia tovuti na njia nyingine za mawasiliano.” anasema Gondwe.



***Afisa Habari na Mkufunzi wa Tovuti za Mikoa na Halamshari kutoka Manispaa na Mtwara Mikindani Jamadi Omari akitoa mafunzo juu ya uandishi wa habari katika tovuti katika moja ya mafunzo yaliyofanyika mkoani Mara (Picha: Jacqueline Sombe , PS3)***

Gondwe anaongeza kuwa, idadi ya watembeleaji wa tovuti imekuwa ikiongezeka siku hadi siku hadi kufikia kiwango cha watu 4000 kwa mwezi Juni, 2019 *(tarehe 27/6/2019)* hali hiyo haijawahi kutokea toka kuundwa na kuanza kutumika kwa tovuti hiyo ya http://dodomacc.go.tz/

“Zaidi ya hapo, GWF imewasaidia pia wanahabari kupata habari na taarifa sahihi kutoka tovuti ya Jiji. Zipo habari nyingi ambazo zimekuwa zikichapishwa katika vyombo vingine vya habari ambavyo chanzo chake ni tovuti ya Jiji. Nadhani kutokana na tovuti kuwa chombo kinachoaminika na kutoa taarifa sahihi na kwa wakati,” anasisitiza Gondwe.

Sekela Mwasubila, Afisa Habari Halmashauri ya Mji wa Kondoa, anasema “Tovuti ni nzuri sababu zinarahisisha kupata habari nyingi za maeneo husika kwa wakati mmoja na hasa kile kinachoendelea ndani ya Halmashauri zetu.


Maoni haya ya Maafisa kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa, yanachagizwa na matamanio ya awali kabisa ya wananchi, Mmoja wa wananchi hao aliyewahi kuhojiwa ni Bwana Chande Athumani wa Mtwara Mikindani, mapema Mwezi Machi, 2017 alinukuliwa akielezea kufurahishwa kwake na taarifa za kuwepo kwa tovuti hizo, na kudai kuwa hapo awali ilikuwa ni vigumu kupata taarifa muhimu ambazo wananchi walizihitaji.

“Tunaamini kuanza kutumika kwa tovuti hizi upatikanaji wa taarifa mbalimbali

***Inaendelea uk. 11***

## ♦ *Je, Tovuti za Mikoa, Halmashauri ni Majokofu au Magofu ya Habari?*

***Inatoka uk. 10***




***Mchoro unaoonesha kiwango cha uwekaji wa habari katika Tovuti za Mikoa 26 ya Tanzania Bara kutoka katika nyenzo ya tathimini 'GWF Monitoring tool' inayosimamiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI (Mchoro: OR– TAMISEMI)***

kama vile namna ya kuweza kupata taarifa ya kulipia leseni na kukata bima kupitia viunganishi vya haraka na kupata maelekezo na huduma mbalimbali tunazozihitaji wananchi kutoka katika Halmashauri zetu, utakuwa umerahisishwa sana. Tunatumaini wananchi hatutalazimika kufuata fomu hizo ofisini, isipokuwa tutakuwa tunazitoa kwenye mtandao,"alinukuliwa Chande.

Tanzania iliweka saini Azimio la '*Open Government Partnership*' mwaka 2011 kuweka uwazi wa shughuli za Serikali kwa wananchi, ikiwa na lengo la kuimarisha utawala bora, kuondoa rushwa na kujenga imani kwa wananchi wake. Azimio linaweka msisitizo kwa wananchi kupata taarifa kwa wakati na uhuru zaidi, hivyo azma ya Serikali kuunda tovuti za Mikoa na Halmashauri ilikuwa ni moja ya juhudi katika kuwafikia wananchi kwa uwazi zaidi.

Katika kudhihirisha kuwa tovuti hizo si magofu tena bali ni majokofu ya habari kama kauli ya Waziri wa Habari Sanaa, Michezo na Wasanii Dkt. Harison Mwakyembe, hali ya uwekaji wa taarifa za msingi kwa manufaa ya umma umekuwa ukiongezeka siku hadi siku, mathalani uwekaji wa habari tu kwenye tovuti kwa kipindi cha miezi 3 iliyopita ilikuwa na habari 300, matangazo 21, matukio 9, na Machapisho tofauti tofauti 14.

Ushahidi endapo tovuti ni Jokofu au gofu unapatikana kupitia nyenzo ya tathmini ijulikanayo kama *GWF Monotoring tool,* ambayo ina uwezo wa kubaini taarifa zilizopandishwa katika Tovuti na kuweza kutambua Mkoa au Halmashauri kuanzia inayoongoza katika kupandisha taarifa hadi ile inayofanya vibaya katika uwekaji wa taarifa. Katika kipindi cha miezi mitatu Mkoa wa Simiyu umeonekana kuwa kinara wa uwekaji wa habari ambapo jumla ya habari 47 zilipandishwa katika tovuti ya Mkoa huo, ilihali Mkoa wa Mwanza ukishika nafasi ya pili kwakuweka habari 39 na Mkoa wa Shinyanga wenyewe uliweza kupandisha habari 23 Mikoa hii kwa Lugha rahisi unaweza kusema imezingatia dhana ya utawala bora.

Kwa upande wa Halmashauri, Manispaa ya Songea imeonekana kuwa kinara wa uwekaji wa taarifa miongoni mwa halmashauri 185 hususani katika ukurasa wa habari kwani ndani ya miezi mitatu jumla ya habari 139 zilipandishwa katika tovuti hiyo, wingi huu wa habari ni kiashiria tosha kwamba tovuti ya Songea Manispaa sio Gofu bali Jokofu la habari mpya mpya, wakati Manispaa ya Songea ikiwa kinara wa uzalishaji wa habari Halmashauri ya Jiji la Arusha imeshika nafasi ya pili kwakupandisha habari 126 na Halmashauri ya Karatu kushika nafasi ya tatu kwakuweka habari 82.

Hata hivyo, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa Ushirikiano na wadau wa Maendeleo nchini USAID chini ya Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) imefanikiwa kufanya ufuatiliaji kwa tovuti zote 211 za Mikoa na Halmashauri, ambapo toka kuanza kutumia nyenzo ya ufuatiliaji inaonesha jumla ya Habari 1571 zimewekwa katika tovuti, Mikoa ikiwa imeweka Habari 303, Halmashauri 1255, hii ni kwa kipindi cha Aprili hadi Julai, 2019.

Yatosha kusema safari ni hatua, kama zisingekuwepo tovuti hizi je? Habari hizi ambazo tumeona zimewekwa kwa manufaa ya umma katika tovuti na kuondosha maswali yasiyokuwa ya msingi yatosha kusema Tovuti sasa ni Jokofu na sio Gofu, lakini kwa upande wa pili kila Mkoa na kila Halmashauri inapaswa kujipima kwa haki ili kuona kama kweli wanatekeleza dhana ya Utawala Bora kwani uwekaji huu wa taarifa nyingi zinazowahusu wananchi kwa wakati unaongeza pia shauku ya watembeleaji kutembelea tovuti hizi.

***Atley Kuni– TAMISEMI***

# Nukuu kutoka Dawati la Wataalam



Wataalamu kutoka Idara ya Afya, Elimu,Mipango,Mazingira na TEHAMA Halmashauri ya Mji Njombe, wakiandaa mpango wa bajeti wa Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2019/2020 katika ukumbi mdogo wa Halmashauri ya Mji Njombe.

"Kwenye PlanRep ya awali, Idara ya Mipango ndio ilikuwa inaingiza *Cost Centre* za kila Idara na Kitengo jambo ambalo lilikuwa linafanya mchakato wa bajeti kuwa mrefu hadi kukamilika kwake, lakini sasa wamebakiwa na shughuli za kubwa ya uratibu na kugawa Ukomo wa bajeti *(Ceiling)* pamoja na kusimamia miongozo ya kila Idara na Vitengo katika uandaaji wa bajeti. Anasema Shigela na kuongeza kuwa, "sasa kuna uwazi na kila mtu anaweza kuingia kwenye mfumo na kuandaa bajeti ya Idara na Kitengo chake, na kama imetokea suala limesahaulika ni rahisi kukumbushana kwakuwa bajeti hufanywa na jopo la watumishi kutoka Idara zote."

**Afisa Mipango Mji wa Njombe Shigella Ganga**

"Kupitia PlanRep iliyoboreshwa, tumeweza kuwajengea uwezo watu wengi katika maeneo yao ya kazi, hususani wale wanaofanya kazi katika vituo vya afya ngazi ya msingi. Kuanzia 2017 Julai, pia tulianzisha utaratibu wa upelekaji wa fedha moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma za afya (DHFF), hii ilikuwa moja ya maboresho yaliyotakiwa kuendana na matumizi ya mipango na bajeti katika PlanRep iliyoboreshwa, na kupitia hili tumewajengea uwezo wa kuandaa mipango na matumizi ya fedha yameimarika, vilevile kupita PlanRep iliyoboreshwa, Mganga Mkuu wa Halmashauri anaweza kuunganisha mipango ya vituo vyote vya afya ngazi ya msingi katika eneo lake, na kuzipeleka mikoani kwajili ya mapitio kisha mkoa kupeleka ngazi ya ofisi za TAMISEMI kwaajili ya mapitio. Haya ndio mafanikio makubwa tuliopata kwenye PlanRep iliyoboreshwa."



**Dkt. Ntuli Kapologwe– Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe Ofisi ya Rais TAMISEMI**